TANGAZO LA SERIKALI NA 186 la Tarehe 06/03/2020

SHERIA YA SERIKALI ZA MITAA (MAMLAKA ZA WILAYA)
(SURA YA 287)

______

# SHERIA NDOGO

______

*Zimetungwa chini ya kifungu cha 153(1)*

______

SHERIA NDOGO ZA (HIFADHI YA MAZINGIRA) ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA MOSHI, 2020

Jina la sheria

1. Sheria Ndogo hii zitaitwa Sheria Ndogo za (Hifadhi ya Mazingira) za Halmashauri ya Wilaya ya Moshi ya Mwaka 2020.

Matumizi

2. Sheria Ndogo hii zitatumika katika eneo lote la Mamlaka ya Halmashauri ya Wilaya ya Moshi.

Tafsiri

3. Katika Sheria Ndogo hii isipokuwa itakapoelezwa vinginevyo:-

"Afisa Mwidhiniwa" Maana yake ni Afisa wa Halmashauri aliyeteuliwa na Mkurugenzi kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi.

"afisa afya" Maana yake ni Afisa wa Afya aliyeajiriwa na Halmashauri ya Wilaya ya Moshi.

"ardhi hatari" Maana yake hi ardhi ambayo ikiendelezwa inaweza kuleta hatari katika maisha au kusababisha uharibifu wa mazingira katika ardhi hiyo au nyingine iliyo karibu.

"chukizo" Maana yake ni kitu chochote kinachoweza kuleta madhara au kuhatarisha afya ya binadamu.

"chakula" Maana yake ni kitu chochote kinachofaa kuliwa na binadamu.

"Halmashauri" Maana yake ni Halmashauri ya Wilaya ya Moshi.

"Mamlaka" Maana yake ni mamlaka ya Halmashauri ya Wilaya ya Moshi.

"Mkurugenzi" maana yake ni Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Moshi pamoja na Afisa yoyote wa umma aliyeteuliwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi;

"Taka hatari" Maana yake ni taka ngumu, miminika na hewa ambazo zina kiwango kibubwa cha kemikali ambazo husababisha sumu na kuathiri maisha ya binadamu pamoja na mazingira kwa ujumla wake.

Wajibu wa Halmashauri katika Mazingira na Vyanzo vya Maji.

4.(1) Halmashauri itakuwa na jukumu la kuhakikisha kwamba:-

(a) inatenga eneo maalum kwa ajili ya kuotesha miche ya miti ambayo itapandwa katika maeneo mbalimbali ndani ya Halamashauri kwa utaratibu utakaopangwa;

(b) Inatenga eneo au maeneo kwa ajili ya kupanda miti au kutunza miti iliyokwisha pandwa kama hifadhi ya misitu na hakuna shughuli zozote zitakazo ruhusiwa kufanyika katika eneo au maeneo hayo;

(c) inasimamia utunzaji wa miti na misitu iliyomo katika mamlaka yake;

(d) inasimamia kampeni za kitaifa, kimkoa na kiwilaya za kupanda miti;

(e) inapanga siku moja au zaidi kwa kila mwaka kwa ajili ya kupanda miti na watu wote wanaopaswa kushiriki katika upandaji huo wa miti watatakiwa kushiriki katika zoezi hilo na watalazimika kufanya hivyo;

(f) inaweka utaratibu mzuri wa kukomesha aina zote za mifugo kuzurura mitaani ili kuepusha uharibifu wa miti iliyooteshwa.

(2) Kila asasi na taasisi zilizomo ndani ya Halmashauri zitahakikisha kwamba:-

(a) zinapanda na kutunza miti katika maeneo yaliyo chini ya uangalizi wao.

(b) zinashiriki vema katika shughuli za kupanda miti pale wanapotakiwa kufanya hivyo.

(c) zinatoa taarifa mara moja kwa mamlaka inayohusika pale inapobainika kumetokea uharibifu wa miti katika maeneo yao.

Zuio la ukataji miti holela.

5.—(1) Ni marufuku kwa mtu yoyote kukata mti au sehemu ya mti pasipo kupata kibali cha Halmashauri.

(2) Halmashauri itatenga maeneo ya misitu ambayo miti itaruhusiwa kukatwa kwa ajili ya matumizi mbali mbali baada ya kupata kibali cha Halmashauri.

Upandaji miti.

6. Mmiliki yoyote wa ardhi atawajibika kupanda na kuhifadhi miti isiyopungua mitano katika eneo lake.

Ardhi hatari.

7. Kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii maeneo ambayo ni vyanzo vya maji, pembezoni mwa mito, visima vya maji, chemichemi za maji pamoja na miteremko ya milima ni maeneo ya ardhi hatari.

Makosa.

8. Itakuwa ni kosa kwa mtu yoyote kufanya shughuli zifuatazo katika maeneo yaliyoainishwa katika kifungu cha 7 hapo juu bila kupata kibali cha Halmashauri:-

(a) kuwasha moto kufanya au kutokufanya jambo lolote ambalo litasababisha moto katika maeneo ya misitu;

(b) kuweka, kujenga, kurekebisha, kuondoa au kubomoa aina yoyote ya jengo;

(c) kuchimba au kulima maeneo ya barabara au pembezoni mwa barabara kwa madhumuni yoyote yale;

(d) kuchepusha maji ya mto au mfereji kutoka katika mkondo wake.

Shughuli za kilimo na hifadhi ya Ardhi.

9.(1) Itakuwa ni wajibu wa kila mkulima kuzingatia kanuni za kilimo bora ili kulinda hifadhi ya ardhi na kuongeza tija katika uzalishaji wa mazao mbalimbali ya kilimo na biashara.

(2) Mtu yoyote atakayebainika kufanya yafuatayo atakuwa ametenda kosa:-

(a) kulima bila kuzingatia kanuni za kilimo bora;

(b) kufanya usindikaji wa mazao mbalimbali kinyume na utaratibu;

(c) bila sababu za msingi kushindwa kutoa taarifa ya milipuko katika Mamlaka husika kuhusu wadudu, ndege au wanyama waharibifu ikiwa ni pamoja na magonjwa kama vile; kweleakwelea, batobato kali na mnyauko;

(d) kubadilisha zao bila kuzingatia taratibu za kitaalamu.

Uharibifu na mmomon-yoko wa ardhi.

10.—(1) Ili kuzuia uharibifu wa na mmomonyoko wa ardhi itakuwa ni marufuku kwa mtu yoyote kuchimba udongo, mchanga na kokoto kwa ajili ya matumizi yoyote yale pasipo kupata kibali cha Halmashauri.

(2) Mtu yoyote atakayepewa kibali cha kuchimba udongo, mchanga au kokoto ataruhusiwa kufanya shughuli iliyokusudia tu na kwa kiasi kilichoainishwa katika kibali husika.

Shughuli za mazishi.

11. (1) Kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii shughuli zote za mazishi zitafanyika katika maeneo yaliyotengwa na Halmashauri au taasisi mbalimbali baada ya kupata kibali kutoka Halmashauri ili kutenga maeneo kwa ajili ya shughuli hiyo.

(2) Mtu yoyote atakayebainika kuhusika katika kufanya shughuli za mazishi katika makaburi yaliyofungwa au katika maeneo ya makazi au maeneo yasiyoruhusiwa kisheria atakuwa ametenda kosa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii.

Shughuli hatarishi kwa hifadhi ya mazingira.

12.—(1) Hakuna mtu yoyote atakayeruhusiwa kukata eneo lolote la barabara pasipo kwanza kupata kibali cha Halmashauri na kulipa ada iliyowekwa kisheria.

(2) Mmiliki yoyote wa ardhi atakuwa ametenda kosa endapo ataruhusu ardhi anayomiliki kwa nia ya kuchimbwa ili kupata udongo, mchanga au kokoto pasipo kupata kibali cha Halmashauri.

(3) Itakuwa ni ukiukwaji wa Sheria hii endapo mtu yoyote atabainika kutumia ardhi kwa matumizi ambayo ni kinyume

na masharti ya matumizi ya kiwanja alichopewa kisheria au eneo hilo.

4.(a) Ili kuepuka uharibifu unaoweza kujitokeza maeneo ya vituo vya mabasi, barabarani na maeneo mengine ya wazi itakuwa ni kosa chini ya Sheria Ndogo hii kutengeneza magari au shughuli yoyote inayohusiana na gari katika maeneo hayo;

(b) Mtu yoyote atakayepatikana na hatia kwa kuvunja Sheria Ndogo hii pamoja na adhabu nyingine atakayopewa pia atalazimika kulipa fidia kutokana na uharibifu aliousababisha.

Udhibiti wa uchafuzi wa hewa.

13. Ili kuepuka madhara ambayo binadamu anaweza kupata kutokana na hewa chafu ni marufuku mtu yoyote kufanya shughuli yoyote inayoweza kuzalisha moshi na hewa chafu katika maeneo ya makazi, maeneo ya wazi na barabarani.

Wajibu wa Wamiliki wa viwanda.

14. Mmiliki yeyote wa kiwanda atahakikisha kuwa:-

(a) anakagua mashine zake mara kwa mara ili kuona kuwa zinafanya kazi vizuri ili kuzuia moshi na hewa chafu;

(b) Mmiliki wa gari ahakikishe gari yeyote inayobeba vifaa vya ujenzi au taka itokanayo na vifaa vya ujenzi kama mchanga, kokoto na pumba za mbao inakuwa katika hali ya kufunikwa; na

(c) Mabomba ya kutolea moshi na hewa chafu yanafungwa vifaa maalum ili kuepuka au kupunguza madhara kwa viumbe hai na mazingira.

Shughuli za gereji na endeshaji wa mashine za kusaga.

15. Shughuli zote za gereji pamoja na mashine za kusaga na za mbao zitafanyika tu katika maeneo yaliyotengwa kwa kazi hiyo ili kuepusha kelele na uzalishaji wa hewa chafu katika maeneo ya makazi.

()

16. Ni marufuku kupitisha magari na pikipiki itoayo kelele katika maeneo yanayohitaji utulivu, hasa katikati ya mji na katika mahospitali; ofisi na taasisi mbalimbali.

Marufuku ya kelele

17. Kila mkazi wa Halmashauri atahakikisha kwamba nyumba yake inakuwa na:-

Ujenzi wa nyumba bora.

(a) milango na madirisha ya kutosha ili kuruhusu hewa na mwanga;

(b) mfumo bora wa kupitisha moshi kutoka jikoni na maeneo mengineyo yanayotoa au kuzalisha moshi;

(c) Kuta na paa zilizo katika hali nadhifu.

18.(a)Itakuwa ni wajibu wa mmiliki, mpangaji wa nyumba kufagia na kuondoa uchafu au marundo ya uchafu na kuweka safi eneo lote la nyumba yake

Wajibu wa kutunza usafi

(b) Vichochoro vyote vitatunzwa na wenye nyumba husika na kila mwenye nyumba au mpangaji atawajibika kutunza eneo lake yaani hatua za upande wake baada ya vigingi vinavyotenganisha viwanja katika uchochoro.

(c) Halmashauri au mtu yeyote aliyeteuliwa kuwa wakala atakuwa na uwezo wa kukusanya, kuhifadhi, kusafirisha na kutupa taka za majumbani na biashara kwa kutoza ada kama ilivyoainishwa katika Jedwali la kwanza.

(d) Kamati za maendeleo za mitaa na kata zitakuwa na uwezo chini ya Sheria Ndogo hizi kusimamia usafi kwenye maeneo yao kwa kukomesha utupaji taka ovyo na usafishaji wa vichochoro.

(e) Kamati za maendeleo za kata na mitaa zitakuwa na uwezo wa kuunda vikosi kazi vya kudhibiti uchafuzi wa mazingira kwa kushirikiana na kamati za afya za kata au mtaa.

19. Mtu yoyote atakayekiuka masharti ya Sheria Ndogo hizi atakuwa ametenda kosa na iwapo atapatikana na hatia atatozwa faini isiyozidi shilingi laki tatu (Tsh. 300,000/=) au kifungo kisichozidi miezi kumi na mbili (12) jela au yote kwa pamoja.

Adhabu.

Kufililisha kosa.

20. Mkurugenzi atakuwa na uwezo wa kufilililisha kosa iwapo mkosaji atakiri kwa maandishi kwa kujaza fomu maalum itakayoambatishwa katika Jedwali la Pili la Sheria Ndogo hii na kulipia faini kiasi kisichozidi shilingi laki mbili (Tsh. 200,000).

JEDWALI LA KWANZA

*(Limetungwa chini ya kifungu cha 18(c))*

SEHEMU "A"

ADA ZA UZOAJI TAKA NGUMU

| Na. | AINA YA BIASHARA | TOZO |
|---|---|---|
| 01. | Maeneo ya Kaya | 500/= kwa wiki |
| 02. | Tea room | 5000/=kwa wiki |
| 03. | Café | 500/= kwa wiki |
| 04. | Restaurant | 1,000/= kwa wiki |
| 05. | Nyumba za wageni | 5,000/= kwa mwezi |
| 06. | Dispensary(normal refuse) | 5,000/= kwa mwezi |
| 07. | Health centre(normal refuse) | 7,000/= kwa mwezi |
| 08. | Viwanda vidogo/garage | 2,000/= kwa mwezi |
| 09. | Hotel: vyumba 01 – 10 | 10,000/= kwa mwezi |
| 10. | Hotel: vyumba 11 – 20<br>Hotel: vyumba 21 – 30<br>Hotel: vyumba 31 – 40<br>Hotel: vyumba 41 – 50<br>Hotel: vyumba 51 – 60 | 15,000/= kwa mwezi<br>20,000/=kwa mwezi<br>25,000/=kwa mwezi<br>30,000/= kwa mwezi<br>35,000/= kwa mwezi |
| 11. | Maduka ya dawa muhimu | 10,000/= kwa mwezi |
| 12. | Bucha | 5,000/= kwa mwezi |
| 13. | Masoko kwa chumba(stals) | 500 /=kwa wiki |
| 14. | Magenge | 500/=kwa wiki |
| 15. | Wauza vyakula mitaani | 500/=kwa wiki |
| 16. | Magari ya mizigo (cargo) | 15,000/= kwa mwezi |
| 17. | Biashara ndogondogo | 500/= kwa wiki |
| 18. | Saloon/vinyozi | 2,000/= kwa wiki |
| 19. | Vituo vya mafuta | 20,000/= kwa wiki |
| 20. | Wauza mikaa | 1,000/= kwa wiki |
| 21. | Maduka ya jumla | 10,000/= kwa mwezi |

| | | |
|---|---|---|
| 22. | Maduka ya vyakula (Super Markets) | 15,000/= kwa mwezi |
| 23. | Maduka ya Hardware | 20,000/=kwa mwezi |
| 24. | Maduka ya rejareja | 10,000/= kwa mwezi |
| 25. | Maabara | 3,000/= kwa wiki |
| 26. | Furniture/carpentry | 5,000/= kwa wiki |
| 27. | Video show | 3,000/= kwa wiki |
| 28. | Battery charge | 1,000/= kwa wiki |
| 29. | Refregerate services | 2,000/= kwa wiki |
| 30. | Welding | 2,500/= kwa wiki |
| 31. | Posho mills | 7,000/= kwa mwezi |
| 32. | Pombe shop | 3,000/= kwa mwezi |
| 33. | Ushonaji nguo | 5,000/= kwa mwezi |
| 34. | Wachoraji | 1,000/= kwa wiki |
| 35. | Soda (whole sale) | 10,000/= kwa mwezi |
| 36. | Studio | 3,000/= kwa mwezi |
| 37. | Spare parts | 5,000/= kwa mwezi |
| 38. | Mafuta ya taa mitaani | 1,000/= kwa wiki |
| 39. | Karakana | 5,000/= kwa mwezi |
| 40. | Bakeries | 5,000/= kwa mwezi |
| 41. | Kuuza magazeti | 1,000/=kwa wiki |
| 42. | Computer services | 3,000/= kwa mwezi |
| 43. | Godowns | 5,000/= kwa mwezi |
| 44. | Stores | 3,000/= kwa mwezi |
| 45. | Uuzaji samaki | 2,000/= kwa mwezi |
| 46. | Mabasi express/taxi (michomoko) | 2,000/= kwa mwezi |
| 47. | Night club | 10,000/= kwa mwezi |
| 48. | Makanisa | 3,000/= kwa mwezi |
| 49. | Miskiti | 3,000/= kwa mwezi |
| 50. | Maduka makubwa ya dawa (pharmacy) | 15,000/= kwa mwezi |
| 51 | Grocery | 5,000/= kwa mwezi |
| 52. | Baa | 10,000/= kwa mwezi |
| 53. | Waosha magari | 2,000/= kwa mwezi |
| 54. | Viwanda(taka Nzito) kwa tani | 5,000/= kwa wiki |
| 55. | Hospitali<br>vitanda 1 – 10<br>vitanda 11 – 20<br>vitanda 21 – 30<br>vitanda 31 – 40 | <br>5,000/= kwa mwezi<br>8,000/= kwa mwezi<br>10,000/= kwa mwezi<br>15,000/= kwa mwezi |

| | | |
|---|---|---|
| | vitanda 41 – 50 | 17,000/= kwa mwezi |
| | vitanda 51 – 60 | 20,000/= kwa mwezi |
| | vitanda 61 – 70 | 25,000/= kwa mwezi |
| | vitanda 62 – 81 | 30,000/= kwa mwezi |
| | vitanda 81 – 90 | 35,000/= kwa mwezi |
| | vitanda 91 – 100 | 50,000/= kwa mwezi |
| | vitanda 101 na kuendelea | 60,000/= kwa mwezi |
| 56 | Magari yaliyobeba watalii kuingia mbuga za wanyama au maeneo ya utalii; | |
| | (a) magari madogo | 5,000/= kwa siku |
| | (b) magari makubwa | 10,000/= kwa siku |

SEHEMU "B"
ADA ZA UNYONYAJI WA MAJI TAKA

| S/N | AINA YA BIASHARA | KIASI KWA SAFARI MOJA(Trip) |
|---|---|---|
| 01 | Nyumba ya kuishi | 15,000.00 |
| 02 | Taasisi | 30,000.00 |
| 03 | Viwanda | 100,000.00 |
| 04 | Kukodi gari nje ya Wilaya | 150,000.00 |

SEHEMU "C"
ADA YA UKAGUZI

| Na. | Aina | kiasi |
|---|---|---|
| i | Hotel | 50,000 kwa mwaka |
| ii | Mgahawa au baa | 30,000 kwa mwaka |
| iii | Nyumba za kulala wageni | 30,000 kwa mwaka |
| iv | Viwanda | 100,000 kwa mwaka |
| v | Biashara nyinginezo | 10,000 kwa mwaka |
| vi | Ukaguzi wa dharura | 15,000 kwa mwaka |

SEHEMU "D"

ADA YA KUPULIZIA DAWA ZA WADUDU

(i) Ada ya kupulizia dawa ya wadudu (fumigation) ambayo itafanywa na Halmashauri

Shs. 3,000/= kwa mita za mraba za eneo (per square meter)

(ii) Ada ya usimamizi wa kunyunyizia dawa ya wadudu unaofanywa na watu binafsi shs. 3,000/= kwa kazi.

SEHEMU "E"

ADA YA MAGARI YA KUMWAGA TAKA DAMPO

| Na. | Aina | kiasi |
|---|---|---|
| a | Gari ujazo wa tani moja | 5,000 kwa tripu |
| b | Gari ujazo wa tani zaidi ya moja | 10,000 kwa tripu |

JEDWALI LA PILI

*(Limetengenezwa chini ya kifungu cha 20)*

HATI YA KUFILILISHA KOSA

Mimi ....................................................................... nakiri KWA HIARI YANGU MWENYEWE mbele ya......................................................... ambaye ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Moshi kwamba tarehe ..........ya mwezi .................. Mwaka................ nilitenda kosa la kukiuka masharti ya kifungu cha …….. cha Sheria Ndogo ya Hifadhi ya Mazingira ya Wilaya ya Moshi ya Mwaka 2019.

Kwa Mamlaka aliyopewa Mkurugenzi wa Halmashauri niko tayari kulipa kiasi cha shilingi laki mbili badala ya kushtakiwa Mahakamani.

NATHIBITISHA KWAMBA MAELEZO HAPO JUU NI YA KWELI NA NIMEYATOA KWA HIARI YANGU KADRI YA UFAHAMU WANGU

Leo tarehe ......................ya Mwezi ................................Mwaka …..............…

Jina: .....................................................

Saini: ...................................................

Mbele ya:-

Jina……...............................................

Cheo: ..................................................

Saini: .................................................

Tarehe: ..............................................

Nembo ya Hlmashauri ya Wilaya ya Mpimbwe imebandikwa kwenye Sheria Ndogo hizi kufuatia azimio lililopitishwa kwenye Mkutano wa Halmashauri uliofanuyika mnamo tarehe 26/01/2018 mbele ya:-

Erasto N. Kiwale
*Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya Wilaya ya Mpimbwe*

L.S

Nyansongo M. Serengeti
*Mwenyekiti Halmashauri ya Wilaya ya Mpimbwe*

NAKUBALI

Dodoma
8 Feburuary, 2020

Mh. Selemani S. Jaffo (MB)
*Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais - TAMISEMI*